

Jina la Mradi:	Mradi wa Misitu ya Jamii – MJUMITA (Lindi)
Eneo Ulipo Mradi:	Wilaya ya Lindi Vijijini na Manispaa ya Lindi, Mkoa wa Lindi, Tanzania
Mmiliki wa Mradi:	Wamiliki ni wengi (Halmashauri za Vijiji) Wakiwakilishwa na MJUMITA
Mhusika:	Rahima Njaidi, Mkurugenzi Mtendaji, MJUMITA
Barua-pepe na Simu:	rnjaidi@gmail.com +255 22 2669007
Mkaguzi:	SCS Global Services
Mhusi wa Ukaguzi:	Francis Eaton, Mratibu, Greenhouse Gas Verification, Natural Resources Division, SCS Global Services
Barua-pepe na Simu:	FEaton@scsglobalservices.com +1 510 452 8027
Muda wa Kuanza kwa Mradi:	Tarehe ya 1 Aprili, 2010
Muda wa Kupunguza Hewa Ukaa:	Miaka 30, Tarehe ya 21 Aprili 2012 - Aprili 20' 2042
Muda wa Mradi:	Tarehe ya 1 Aprili 2010 na utaendelea hadi Aprili 20 2042
Uthibitishaji Uliokamilika kwa Kutumia Viwango vya CCB Toleo la 3	
Historia ya Kuthibitishwa na CCB:	Uthibitishaji wa Kwanza
Tarehe ya Kukamilika kwa Andiko hili la Mradi:	Tarehe 18 Aprili 2014
Utaratibu wa Uhakiki Unaotegemewa:	Uhakiki wa awali utafanyika pamoja na uthibitishaji wa awali. Uhakiki wa baadaye utafanyika kwa mujibu wa VCS kwa kila kipindi cha miaka 1 – 2.

MUHTASARI WA MATARAJIO YA MRADI KUHUSU MANUFAA KWA TABIANCHI, JAMII NA BIOANUWAI

Kwa kufanya kazi katika maeneo yenye wingi wa bioanuwai yalioko misitu ya ukanda wa Pwani mwa Afrika ya Mashariki ya, mradi huu wa jamii utatekeleza malengo yafuatayo:

Tabianchi

- Kupunguza uzalishaji wa gesijoto zinazotokana na ufyekaji wa misitu katika ardhi ya vijiji kwa kupitia usimamizi endelevu wa misitu.
- Kuongeza kiwango cha hewa ukaa katika misitu ya hifadhi ya vijiji kwa kuendeleza ukuaji wa asili wa misitu.

Jamii

- Kudumisha huduma za mfumo ikolojia wa msitu na upatikaji endelevu wa mazao ya misitu kupitia usimamizi shirikishi wa misitu ulio madhubuti na wenye usawa.
- Kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja kutokana na MKUHUMI kwa kuwekeza katika shughuli za kilimo bora na shughuli nyingine za kiuchumi kwa kuboresha hali ya ujumla ya maisha na kulenga zaidi kaya maskini na akina mama.
- Kuongeza ubora na upatikanaji wa huduma za jamii na miundombinu.

Bionuwai

- Kuhifadhi aina za viumbe vilivyo katika tishio na hatari ya kutoweka.
- Kuhifadhi eneo la nyongeza la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

Mradi utatekelezwa na jamii kutoka vijiji kumi kwa kuanzia ukiwa na uwezekano wa kuongeza vijiji vingine katika ukanda wa mradi siku za usoni kwa kufuata mfumo wa programu.

Kigezo cha Kiwango cha Dhahabu

Mradi una dhumuni ya kufikia kigezo cha kiwango cha dhahabu:

GL 1: Manufaa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi: Mradi utaongeza uwezo wa wakulima wadogo kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha fedha za miradi ya maendeleo ya jamii kama huduma za afya, miundombinu ya ukusanyaji na usambazaji wa maji ambayo itapunguza hali hatarishi kwa jamii kwa kiwango cha kuongeza uhimili kwa magonjwa na upungufu wa maji ambao umebashiriwa katika eneo hili kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa kuanzisha usimamizi wa misitu ya jamii na kuboresha mbinu za kilimo, mradi utalinda thamani ya bioanuwai dhidi ya ongezeko la msukumo kutoka katika kilimo cha kuhama hama kutokana na atahari mbalimbali za mabadiliko ya tabianchi.

GL2. Manufaa ya kipekee kwa jamii: Manufaa kwa jamii ndo kiini cha mradi huu. Usanifu wa mradi umeundwa na wanajamii na jamii ndo wasimamizi kisheria wa eneo lote la mradi. Toka mwanzo wa mradi, mradi ulidhamilia kuonyesha njia rahisi na zenye ufanisi kutekeleza MKUHUMI.

GL 3: Manufaa ya kipekee ya Bioanuwai: Eneo la mradi linajumuisha idadi ya mamalia wadogo ambao wako katika hatari kubwa, Komba wa Rondo ni moja wapo na aina nyingine ya mimea mitatu ambayo iko katika orodha ya aina ya mimea iliyoko hatarini kutokweka ya Shirika la Kimataifa la Uhifadhi na Asili (IUCN). Kwa kulinda makazi ya viumbe hawa mradi unadhamilia kulinda upungufu wa idadi hii katika eneo la mradi.



MKUHUMI Unaotekelezwa na Jamii katika Misituta ya Pwani Tanzania

Andiko la Usanifu wa Mradi (Project Design Document -PDD)

Kwa ajili ya Uihakiki kwa Kutumia Viwango vya Miradi ya Tabianchi, Jamii na Bionuwai (Climate, Community and Biodiversity (CCB) Project Standards)

1) Utangulizi


Kitini hiki kinatoa muhtasari wa lugha ya Kiswahili wa Andiko la Usanifu wa Mradi kwa ajili ya mradi wa 'MKUHUMI Unaotekelezwa na Jamii katika Misituta ya Pwani Tanzania'. Andiko hili linaelezea kuhusu mradi wa MKUHUMI kwa ajili ya wahakiki kutoka nje ya mradi kuja kufanya tathmini kama unakidhi viwango vya Miradi ya Tabianchi, Jamii na Bionuwai (Climate, Community and Biodiversity (CCB) Project Standards) Viwango hivi hutoa mwongozo kwa wanaohusika na kuandaa na kutekeleza miradi namna ya kuhakikisha kuwa miradi ya MKUHUMI inaleta matokeo mazuri (chanya) ya kijamii, kwa ajili ya tabianchi na bionuwai.

G1 Hali halisi ya Eneo Kabla ya Mradi


G 1.1 Mradi Ulipo na Vipimo vya Hali ya nchi

Mradi upo katika Wilaya ya Lindi, Mkoa wa Lindi upande wa Kusini Mashariki mwa Tanzania (angalia Ramani ya 1). Mradi unajumuisha vijiji 10: Kinyope, Kiwawa, Likwaya, Makumba, Milola Magharibi, Mkanga 1, Mkombamosi, Muungano, Nandambi na Ruhoma. Mvua kwa kawaida hunyesha kati ya Novemba na Januari (*vuli*) na kati ya Machi na Mei (*masika*). Wastani wa kiwango cha joto katika Wilaya kinaanzia nyuzi nyoto 24°C hadi 28°C.

Ramani ya 1. Eneo la mradi.



Ramani ya 2. Ramani ya vijiji vya mradi



G 1.2 Uoto wa Asili

Kuna mchanganyiko wa misitu ya ukanda wa nyika katika miinuko ya Chitoa na Noto na miteremko ya Likonde (maeneo yenye ukijani mweusi katika kielelezo cha 1). Misitu ya ukanda wa nyika ya pwani ya Afrika Mashariki ina tabia kadhaa; ina mimea ya aina nyingi; na kuna aina nyingi ya jamii ya mimea ambayo iko hatarini kotoweka na inatishiwa kutoweka. Misitu ya ukanda wa nyika ya pwani imepakana na misitu ya miombo ya pwani kwa upande wa magharibi na mapori mchanganyiko ya misitu kwa upande wa mashariki iliyochanganyikana na maeneo ya kilimo, kilimo mseto, mashamba yaliyopumzishwa na miti inayoendelea kukua.

G 1.3 Mipaka ya Mradi

Mradi una eneo la hekta 41,924 likijumuishwa na eneo lote lenye mapori yenye miti kwa kuanzia mwezi Aprili 2012 katika mipaka ya vijiji 10 vinavyoshiriki katika mradi isipokuwa eneo lililoonekana kuwa siyo msitu mwezi Mei 2001 au lilifyekwa kati ya Mei 2001 na Aprili 2012. Ukanda wa Mradi linajumuisha eneo lote lililo ndani ya mipaka ya vijiji 10 vinavyoshiriki katika mradi wa MKUHUMI.

G 1.4 Kiasi cha Hewa Ukaa

Katika kipindi cha utekelezaji wa mradi, ufekaji wa misitu ulipungua kwa asilimia 29.4% ukilinganisha na hali ya awali ambapo jumla ya hekta 302 hazikufyekwa na kuzuia uzalishaji wa hewa ukaa kwa tani 40,178 kama inavyooneshwa kwenye ramani hapa chini.

G 1.5 Maelezo ya Jamii

Orodha ya Vijiji vinavyoshiriki na Vitongoji.

Kata	Vijiji	Vitongoji
Milola	Milola Magharibi	Jumla: 6 Dodoma B, Kikumbi, Noto, Kipunga, Magela Litandamkumbi
Rutamba	Kinyope	Jumla: 4

Kata	Vijiji	Vitongoji
		Namkopo, Sokoni, Gulioni, Shuleni
	Ruhoma	Jumla: 3 Mchati, Shuleni, Mkundi
Nangaru	Mkombamosi	Jumla: 7 Lumo, Msikitini, Sokoni, Mwenge, Cheleweni, Likonde chini, Likandilo
	Muungano	Jumla: 7 Mnazi Mmoja, Likonde, Kipunga, Uleka, Umoja, Naruwi, Ujamaa
Tandangongoro	Mkanga 1	Jumla: 4 Mandanje, Mkanga Chini, Kilangalamatu, Mkanga Juu
Nga'pa / Tandangongoro	Nandambi	Jumla: 3 Nandambi shuleni, Kilolombwani, Umoja
Matimba	Likwaya	Jumla: 2 Lumumba, Mapinduzi
	Makumba	Jumla: 2 Mapinduzi na Mkwajuni
Kiwawa	Kiwawa	Jumla: 8 Kiwawa B, Kiwawa A, Mchinjidi A, Mchinjidi B, Mmumbu A, Mmumbu B, Nawamba, Kitulo

Idadi ya Watu: Jumla ya idadi ya watu katika vijiji vinavyotekeleza mradi ni 16,051. Hii imeainishwa kwa kila kijiji hapa chini. Takwimu hizi zimetokana na idadi ya watu waliosajiliwa kwa ajili ya malipo ya majaribio ya fedha za MKUHUMI kwa kila kijiji. Wamwera ndio kabila lenye watu wengi zaidi ya asilimia 90 katika vijiji vingi vya eneo la mradi. Ingawa katika kijiji cha Likwaya Wamakonde ndiyo wengi zaidi kwa zaidi ya asilimia 90.

Kijiji	Wanaume	Wanawake	Watoto na Wategemezi	Jumla
Kinyope	963	1348	1596	3,907
Kiwawa	379	441	918	1738
Likwaya	131	167	263	561
Makumba	172	217	281	670
Milola Magharibi	507	541	1,351	2399
Mkanga	196	231	353	780
Mkombamosi	118	639	1508	2,265
Muungano	507	541	1,351	2,399
Nandambi	200	236	295	731
Ruhoma	133	213	255	601
Jumla	3,306	4,574	8,171	16,051

Historia na Utamaduni: Watu wa asili ya Wabantu walianza kuishi Tanzania takribani miaka 2000 iliyopita. Kabla ya mwaka 1974 kaya nyingi zilitawanyika, nyingi zikiwa katika maeneo ya misitu. Katika miaka ya 1960 kilianzishwa Chama cha Ushirika cha Ilulu kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho, ufuta na njegere. Vijiji viwili vya Nandambi na Ruhoma kati ya vijiji vya mradi vilianzishwa wakati wa ujamaa. Kiswahili ndio lugha inayozungumzwa na kueleweka na watu wengi zaidi. Katika vijiji vyote ilibainika kuwa watu wengi zaidi ni Waislam. Ilielezwa pia kuwa Wakristo wachache wapo katika vijiji vyote na baadhi ya imani za jadi zipo katika eneo la mradi. Kwa ujumla, huduma nyingi za jamii/umma katika eneo la mradi hazipo katika baadhi ya vijiji na katika maeneo mengine zipo katika hali isiyo ya kuridhisha.

Usafiri na Mawasiliano: Eneo la mradi linafikika kwa kutumia barabara za udongo zinazolingia na kutoka katika barabara kuu itokayo Kilwa kwenda Mtwara. Shirika la Utangazaji Tanzania (The Tanzania Broadcasting Cooperation – TBC) ndio radio inayosikizwa na jamii nyingi za Lindi. Mawasiliano ya simu yanayopatikana ni ya mitandao ya simu za mkononi. Mitandao ya huduma za simu inayopatikana ni Airtel

(zamani Zain na Celtel), Tigo na Vodacom inayopatikana katika kijiji cha Nangaru. Hakuna kijiji katika eneo la mradi kilichofikiwa na umeme wa gridi ya taifa. Mwanga unapatikana kwa kuwasha taa za chemli na mishumaa.

Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo, ufugaji nyuki kidogo, uvuvi, uchomaji mkaa, na ujasiriamali mdogo. Kilimo cha kuhamahama ni aina kuu ya mfumo wa kilimo unaotekelezwa katika eneo la mradi. Kwa wastani, kila kaya hufyeka eka 1 – 5 sawa na hekta 0.81 – 2.02 za msitu mpya au msitu unaokua kwa ajili ya kuandaa mashamba. Visima vya asili na mikondo ya maji ndiyo vyanzo vikuu vya maji yanayotumika katika kaya nyingi za eneo la mradi.

G 1.6 Matumizi ya ardhi ya sasa na mfumo wa kimila na kisheria wa umiliki mali

Aina za matumizi ya ardhi zinajumuisha maeneo ya kilimo cha kudumu, makazi, huduma za jamii, malisho, misitu ya hifadhi kwa ajili ya matumizi endelevu; misitu ya matumizi; na maeneo na maeneo ya kilimo yaliyochanganyika na makazi msongamano. Kwa ujumla, kuna utaratibu wa wa kutenga maeneo ya mabondeni kwa kwa ajili ya kilimo na makazi wakati misitu inatengwa katika maeneo ya miinuko. Ardhi yote ndani ya mipaka ya kijiji ipo chini ya mamlaka ya serikali ya vijiji. Umiliki wa ardhi wa kimila unatambuliwa kwa ajili ya kilimo cha mazao ya kudumu ya biashara. Maeneo ya misitu, isipokuwa tu kama ipo ndani ya msitu wa hifadhi wa kijiji, yanaonekana kama eneo la wazi linaloweza kubadilishwa na kumilikiwa kimila kwa kufyekwa na kuwa shamba.

G 1.7 Bionuwai ya sasa

Misitu ya Pwani ya Lindi ni sehemu ya Misitu ya Pwani ya Afrika Mashariki yenye wingi wa bionuwai ya pekee. Timu ya watafiti wa bioanuwai (mimea na mamalia wadogo) ya TFCG iligundua mimea 279, mamalia 26 na aina za ndege 36 katika eneo la mradi. Tishio lililopo sasa kwa bionuwai ni pamoja na: kufyekwa kwa makazi, uharibifu wa makazi kutokana na ukataji wa magogo, uchomaji wa mkaa, moto na uwindaji.

G 1.8 Thamani Kubwa ya Uhifadhi

Katika eneo la mradi, kuna misitu ya hifadhi ya vijiji 10 iliyo katika eneo lenye jumla ya hekta 35,021 ya misitu ya Pwani na mapori. Misitu ya miinuko ya Noto-Chitoa ni mifano ya pekee ya misitu ya Pwani ya Afrika Mashariki. Misitu mingine inayobakia katika pwani ya Tanzania haizidi kilometa za mraba 50. Miinuko hii ina zaidi ya kilometa za mraba 350.

Kijiji	Eneo (hekta)
Milola Magharibi	594
Kinyope	1,862
Muongano	5,847
Ruhoma	2,975
Mkombamosi	3,242
Mkanga 1	870
Likwaya	816
Kiwawa	8,352
Nandambi	5,761
Makumba	4,702
Jumla	35,021

Maeneo ya miinuko ni vyanzo muhimu vya maji yanayotiririka kuelekea upande wa mashariki na kutoa maji kwa wakaazi wanaoishi mabondeni.

Kuna aina 19 ya viumbe waliorodheshwa na IUCN kama viumbe adimu walio katika hatari ya kutoweka na aina 6 za viumbe walio katika kundi la kukaribia kuwa hatarini kutoweka.

Aina	Hatari ya kutoweka kabisa	Hatari ya kutoweka	Hatarini	Kukaribia kuwa katika hatari ya kutoweka
Mimea	2	5	9	1

Aina	Hatari ya kutoweka kabisa	Hatari ya kutoweka	Hatarini	Kukaribia kuwa katika hatari ya kutoweka
Mamalia	1		2	2
Ndege				3
Jumla	3	5	11	6

Kuna jumla ya viumbe 25 ambavyo havipatikani sehemu nyingine na vinapatikana katika eneo la mradi wa MKUHUMI tu.

Jedwali 1. Muhtasari wa idadi ya viumbe adimu wanaopatikana katika eneo mradi tu.

Aina	Adimu kwa Lindi	Adimu kwa Misitu ya Pwani	Kukaribia kuwa adimu kwa Misitu ya Pwani
Mimea	8	10	1
Mamalia	0	2	1
Ndege	0	1	2
Total	8	13	4

Chakula na matunda ya pori hukusanywa na wanawake na watoto. Aina ya vyakula vinavyopatikana msituni mara nyingi ni mizizi ya Ming'oko na mipama. Mimea ya dawa za asili hukusanywa na kutumika katika vijiji vyote. Uwindaji mdogo mdogo kwa ajili ya kitoweo hufanyika katika vijiji vyote. Wanyama wanaowindwa mara nyingi ni funo, pongo, ngiri, nyati, tembo na kima.

G1.9. Muda wa Utekelezaji wa Mradi na Ratiba ya Utekelezaji

Tarehe ya kuanza mradi ilikuwa ni Tarehe 1 Aprili 2010 muda ambao timu ya mradi ilianza shughuli za mradi katika wilaya ya Lindi. Hata kama Mradi wa 'MKUHUMI wa Kuwezesha jamii na Uhifadhi wa Misitu Tanzania' ulianza tarehe 1 Agosti 2009, kati ya Agosti 2009 na Machi 2010, mradi uliangalia zaidi uchambuzi na uchaguaji wa maeneo ya kutekeleza mradi na shughuli za kuanza mradi ambazo hazikusababisha manufaa ya moja kwa moja yaliyotegemewa na mradi kuhususiwa na tabianchi, jamii na bioanuwai.

Kipindi cha mradi

Kipindi cha mradi kinaanza tarehe ya kuanza mradi mathalan Tarehe 1 Aprili mwaka 2010 na kitaendelea kwa muda usiojulikana kutokana na kutokuwepo muda maalum wa utekelezaji wa shughuli muhimu za mradi.

Kipindi cha Upataikanaji wa kiasi cha Gesijoto

Kipindi cha upatikanaji wa kiasi cha gesijoto, kitakuwa kutoka tarehe 21 Aprili mwaka 2012 hadi Aprili 20 Mwaka 2042. Tarehe ya kuanza kwa upatikanaji wa kiasi cha gesijoto inaendana na tarehe ya picha ya anga iliyoonekana vizuri ya LANDSAT 7 iliyotumika kutayarishia ramani ya uoto. Angalia Andiko la mradi wa Viwango vya hiari (VCS) kwa taarifa za kina zaidi.

Kipindi cha kutathmini manufaa ya bioanuwai na jamii

Kipindi cha tathmini ya manufaa kwa bioanuwai na kwa jamii ni kipindi cha mradi.

Uthibitishaji wa tofauti kati ya kipindi cha upatikanaji wa gesijoto na kipindi cha kutathmini manufaa ya bioanuwai na jamii.

Shughuli za utayarishaji wa MKUHUMI zilianza tarehe 1 Aprili mwaka 2010 zikiwa ni pamoja na uhamasishaji na shughuli ya uelimishaji na kukubali mradi katika vijiji vyote; utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji, kutayarisha mipango shirikishi wa usimamizi wa misitu, malipo ya majaribio ya MKUHUMI, na mafunzo ya kilimo bora katika baadhi ya vijiji. Hata hivyo, sheria ndogo za matumizi mapya ya ardhi na hifadhi za misitu ya vijiji zilizopitishwa na vijiji vinavyoshiriki zilianza kutumika kuanzia mwaka 2012. Malipo ya kwanza ya majaribio walioyapata yalikuwa ni kwa ajili ya kumalizia mchakato wa shughuli za utayarishaji wa MKUHUMI yalifanyika Novemba 2011. Hivyo basi, mradi usingetegemewa kuwa na athari katika kupunguza uzalishaji wa gesijoto kabla ya mwaka 2012. Kutokana na hili, na kutokana na upatikanaji na utumiaji wa picha za anga, kipindi cha upatikanaji wa gesijoto kilipangwa kuanza tarehe 21 Aprili 2012.

Mpango wa Utekelezaji

Tarehe muhimu na malengo makuu ya mradi zimeelezeka katika mpango wa utekelezaji hapa chini.

Jedwali la 2: tarehe muhimu na malengo makuu katika maendeleo ya mradi.

Tarehe	Malengo makuu katika maendeleo ya utekelezaji wa mradi
Aprili – Mei 2010	Mikutano ya kujitambulisha, shughuli za kuelimishana na kukubali mradi, mafunzo na kuanzisha kwa mfumo wa ufuatiliaji.
Juni – Septemba 2010	Mikutano na wanavijiji katika ngazi ya vitongoji na vijiji kuhusu MKUHUMI. Wanavijiji kukubali kuendelea na mradi na TFCG na MJUMITA kuendelea na shughuli za utayari wa mradi.
Novemba 2011 – Februari 2013	Malipo ya majaribio ya MKUHUMI yalifanyika kwa vijiji vilivyoshiriki katika mradi na kumaliza mchakato wa shughuli za mradi kama mipango ya matumizi bora ya ardhi na mipango ya usimamizi wa misitu.
21 Aprili 2012	Kuanza kwa kipindi cha mradi
Aprili 2013	Kumalizika kwa kipindi cha kwanza cha utekelezaji wa mradi
Julai 2013	Mipango ya usimamizi wa misitu na sheria ndogo; Mipango ya matumizi bora ya ardhi na sheria ndogo; Sheria ndogo za Mgawanyo wa mapato ya MKUHUMI ilipitishwa na kusainiwa na Halmashauri ya Wilaya. Mchakato wa kupitisha na kusaini ulichukuwa zaidi ya miaka miwili kutoka Julai 2011 hadi Julai 2013 wakati mipango mingi ilishapitishwa katika mikutano mikuu ya vijiji kati ya Julai hadi Desemba 2011 na kusainiwa katika ngazi ya Halmashauri mwezi Julai 2013. Kutokana na kwamba Halmashauri ya Wilaya ilipitisha zaidi ya siku 60 zinazoshauriwa katika mchakato wa kuoitisha mipango hii, wanavijiji walianza kutekeleza mipango yao na sheria ndogo mwaka 2012. Taarifa ya kina imetolewa katika sehemu ya CM 2.1 ya Taarifa ya Utekelezaji wa mradi
Mei – Juni 2013	Makubaliano ya Utendaji yalifikiwa baina ya Jamii na MJUMITA na kusainiwa na wanavijiji yakukubali MJUMITA kuendelea na mchakato wa uthibitishaji kwa kutumia Viwango vya Hiari vya Kaboni (VCS) na Viwango vya Tabianchi, Jamii na bioanuwai. (CCB)
Machi 2014	Awamu ya pili ya malipo ya MKUHUMI kwa vijiji vinavyoshiriki
Agosti 2014	Kufanyika kwa Tathmini na Uthibitishaji
Desemba 2014	Awamu ya pili ya malipo ya MKUHUMI kwa vijiji vinavyoshiriki
Agosti 2015	Kufanyika kwa Uthibitishaji wa awamu ya pili
Desemba 2015	Awamu ya tatu ya malipo ya MKUHUMI kwa vijiji vinavyoshiriki
Agosti 2017	Kufanyika kwa Uthibitishaji kwa awamu ya tatu
Desemba 2017	Awamu ya nne ya malipo ya MKUHUMI kwa vijiji vinavyoshiriki
Agosti 2019	Kufanyika kwa Uthibitishaji wa awamu ya nne
Desemba 2019	Awamu ya tano ya malipo ya MKUHUMI kwa vijiji vinavyoshiriki
Agosti 2021	Kufanyika Uthibitishaji kwa awamu ya sita
Desemba 2019	Awamu ya sita ya malipo ya MKUHUMI kwa vijiji vinavyoshiriki kupunguza hewa ukaa

G2 Maoteo ya awali/msingi

G 2.1 Yanayoweza kujitokeza kuhusu hali ya matumizi ya ardhi

Vijiji vyote kasoro kijiji kimoja walieleza kuwa maeneo ya misitu yatafungwa katika kipindi cha miaka 5, 10 na 30 kama mradi wa MKUHUMI hautatekelezwa. Kwa hiyo, kinachoweza kujitokeza kuhusu hali ya matumizi ya ardhi bila mradi wa MKUHUMI ni kuendelea kwa ufyekaji wa msitu kwa ajili ya kilimo cha kuhamahama hususan kilimo cha mahindi. Vitendo vya kukatwa kwa miti ya mbao na magogo iliyobakia vitaendelea kwa kulenga aina mpya ya miti kwa kuwa aina ya miti iliyozoeleka na inayofaa zaidi kibiashara itakuwa imeisha katika eneo la mradi. Ukusanyaji wa kuni na ukataji wa nguzo na miti ya ujenzi utaendelea kuchochea uharibifu wa msitu.

G 2.2 Manufaa ya nyongeza ya mradi

Wanajamii waliulizwa matarajio yanayofikiwa kuhusu mabadiliko ya kijamii yanayoweza (yanayohusu maliasili) kujitokeza kwa muda mfupi (miaka 5), muda wa kati (miaka 10), na muda mrefu (miaka 30) bila kuwepo kwa mradi wa MKUHUMI.

- Bila mradi wa MKUHUMI wanajamii wasingeweza kuwa na usimamizi wa misitu na, kwa kuzingatia historia ya kiwango cha uharibifu wa misitu, katika kipindi cha miaka 30,
- Bila mradi wa MKUHUMI, wanajamii wasingeweza kupokea malipo ya fedha za MKUHUMI. Kwa hiyo, kipato cha kaya nyingi hususani kaya maskini kingetegemea shughuli za kilimo peke yake.
- Bila mradi wa MKUHUMI kungekuwa na kiwango kidogo na kasi ndogo ya kuboresha huduma za jamii na miundombinu katika eneo la mradi.

G 2.3 Mabadiliko ya Kiwango cha Hewa Ukaa 'Bila Mradi'

Ili kukadiria uzalishaji wa Gesi Joto bila mradi (hali ya awali), Mradi ulifuata hatua zilizoidhinishwa katika Kanuni za Viwango vya Hiari vya soko la koboni (VCS methodology VM0015)

Kwa kutumia picha za anga na takwimu za taarifa za kijiografia, mradi uliandaa ukanda rejea wa maeneo ya misitu ikiwemo misitu iliyoko ndani ya eneo la mradi na misitu mingine katika Wilaya ya Lindi and Ruangwa. Umakini ulitumika kuhakikisha kwamba ukanda rejea ulifanana na eneo la mradi hususan visababishi vya ukataji wa miti, muundo wa kijiografia, hali ya kiikolojia na hali ya kijamii na kiuchumi.

Tulipomaliza kuandaa ukanda rejea, uchambuzi wa historia ya ufyekaji wa misitu kutoka mwaka 2001 hadi 2012 ulifanyika ili kujua kiwango cha ufyekaji na mwenendo wa ufyekaji katika eneo la ukanda rejea. Mradi uligundua kwamba wastani wa kiwango cha ufyekaji kwa mwaka katika ukanda huu ni asilimia 1.99.

G 2.4 Huduma za mfumo ikolojia 'Bila Mradi'

Kupungua kwa ukubwa wa eneo la msitu kunapelekea kupungua kwa idadi ya mimea, wanajamii wataona ongezeko la ugumu wa kutafuta uyoga, matunda, mitishamba, majani ya malisho, na mazao ya chakula yanayopatikana msituni yanayotumika sasa. Hali hii itazikabili kaya maskini zaidi na kupelea kuwa na hali ngumu zaidi kwa kuwa ndiyo wanaotegemea zaidi mazao ya misitu. Upatikanaji wa mazao ya mbao na kuni utapungua; mmomonyoko wa ardhi utaongezeka na upatikanaji wa maji utapungua.

G 2.5 Hali ya Bionuwai 'Bila Mradi'

Bila mradi wa MKUHUMI, viumbe ambavyo ni tegemezi kwa misitu vikijumuishwa na vilivyo katika hatari ya kutoweka na ambavyo havipatikani sehemu nyingine watatoweka.

G3 Malengo ya Usanifu wa Mradi

G 3.1 Malengo ya Mradi

Yafuatayo ni malengo ya mradi yaliyobainishwa na wadau.

Tabianchi

- Kupunguza uzalishaji wa gesijoto zinazotokana na ufyekaji wa misitu katika ardhi ya vijiji kwa kupitia usimamizi endelevu wa misitu.
- Kuongeza kiwango cha hewa ukaa katika misitu ya hifadhi ya vijiji kwa kuendeleza ukuaji wa asili wa misitu.

Jamii

- Kudumisha huduma za mfumo ikolojia wa msitu na upatikaji endelevu wa mazao ya misitu kupitia usimamizi shirikishi wa misitu ulio madhubuti na wenye usawa.
- Kuongeza kipato cha mtu mmoja kutokana na MKUHUMI kwa kuwekeza katika shughuli za kilimo bora na shughuli nyingine za kiuchumi kwa kuboresha hali ya ujumla ya maisha na kulenga zaidi kaya maskini na akina mama.
- Kuongeza ubora na upatikanaji wa huduma za jamii na miundombinu.

Bionuwai

- Kuhifadhi aina za viumbe vilivyo katika tishio na hatari ya kutoweka.
- Kuhifadhi eneo la nyongeza la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

Wana jamii walipoulizwa kuhusu kipaumbele cha malengo ya mradi walieleza kuwa kwanza ni usimamizi endelevu wa misitu ikifuatiwa na kuimarisha shughuli za kilimo na kuimarisha huduma za jamii.

G 3.2 Shughuli za mradi

Shughuli za mradi zinaendana na vipaumbele vilivyoainishwa na wanajamii.

Shughuli za mradi zitakazoendelea katika kipindi chote cha mradi yaani hadi ifikapo 2022

- Kuboresha utawala bora katika ngazi za vijiji.
- Kutekeleza mipango endelevu ya usimamizi wa ardhi
- Usimamizi wa misitu ya jamii.
- Malipo ya fedha za MKUHUMI kwa jamii.
- Kuimarisha huduma za jamii na miundombinu.

Shughuli zilizotekelezwa kuanzia 2010 – 2014 kupitia TFCG na MJUMITA zinazotakiwa kuendelezwa na Halmashauri za Wilaya baada ya -2014.

- Kuongeza faida na ikolojia endelevu ya shughuli za kilimo.
- Kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa ajili ya jamii.
- Kutengeneza kipato kutokana na mauzo ya mazao ya nyuki.
- Kuotesha na kuvuna miti katika mashamba ya wanajamii kupitia kilimo mseto.

G 3.3 Mradi Unapotekelezwa

Mradi unatekelezwa katika vijiji nane vilivyo katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi Vijijini, na vijiji viwili vilivyo katika Manispaa ya Lindi.

G 3.4 Muda wa Mradi na Kipindi cha Kupima Gesijoto

Kipindi cha historia rejea ya mradi ni kuanzia Tarehe 25 Mei, 2001 hadi Tarehe 21 Aprili, 2012. Muda wa kwanza utakaowekwa taarifa za awali za kuanza utekelezaji wa mradi rasmi itakuwa ni tarehe 21 Aprili, 2012 hadi tarehe 20 Aprili, 2042.

G 3.5 Tathmini ya tahadhari za hatari

Maelezo ya Tahadhari ya Hatari	Uwezekano wa kutokea na athari za hatari	Namna ya kupunguza uwezekano wa kutokea
Hatari 1. Wawekezaji kununua misitu katika eneo la mradi na kufyeka misitu kwa ajili ya kilimo.	Uwezekano wa kutokea: Mdogo / wa kati Athari zinazoweza kujitokeza kwa mradi : Kubwa	Kuelimisha jamii kuhusu masuala ya haki za ardhi; kuimarisha utaratibu wa umilikishaji wa ardhi kwa wanakijiji kupitia mpango wa matumizi bora ya ardhi, utatuzi wa migogoro ya mipaka; kutoa vyeti vya umiliki wa ardhi ya kijiji na kutoa motisha kwa wanavijiji kwa kuendelea kumiliki maeneo ya ardhi yenye misitu katika vijiji vyao kupitia malipo ya MKUHUMI
Hatari 2. Migogoro ndani ya jamii kuhusu haki za kuingia msituni.	Uwezekano wa kutokea: wa kati Athari zinazoweza kujitokeza kwa mradi : Kubwa	Shughuli za maandalizi ya utekelezaji wa MKUHUMI zilizotekelezwa kwa kufuata na kuzingatia kanuni za kupewa taarifa za kabla na kuwa na uhuru wa kutoa ridhaa au kukataa. Kwa kuwahusisha wadau wengi katika kipindi cha usanifu wa mradi, kuna uungwaji mkubwa wa mkono wa mpango huu kuanzia katika

Maelezo ya Tahadhari ya Hatari	Uwezekano wa kutokea na athari za hatari	Namna ya kupunguza uwezekano wa kutokea
		ngazi ya jamii na kitaifa ukijumuisha Wabunge wa maeneo husika, Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Maendeleo ya Kata.
Hatari 3. Rushwa inayohusiana na malipo ya MKUHUMI kudhoofisha umadhubuti na usawa katika utekelezaji wa MKUHUMI.	Uwezekano wa kutokea: wa kati Athari zinazoweza kujitokeza kwa mradi: ndogo / za kati	Mfumo wa malipo ya MKUHUMI kwa mtu binafsi umeundwa ili kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za malipo ya MKUHUMI.
Hatari 4. Rushwa inayohusiana na usimamizi wa misitu inaweza kupelekea ufyekaji wa misitu	Uwezekano wa kutokea: Mdogo Athari zinazoweza kujitokeza kwa mradi: za kati	Mitandao ya MJUMITA imeundwa katika vijiji na inaendelea vizuri katika kuzuia na kutatua masuala ya ubadhirifu na kuchochea usimamizi endelevu wa misitu.
Hatari 5. Kutokuwepo kwa utashi wa kisiasa kwa ajili ya utekelezaji wa MKUHUMI Tanzania na sheria kuzuia jamii kupata malipo ya moja kwa moja ya fedha za MKUHUMI	Uwezekano wa kutokea: Mdogo Athari zinazoweza kujitokeza kwa mradi : Kubwa	Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji wa MKUHUMI umechapishwa mwaka 2013 na unaelezea utayari wa serikali kuendelea na utekelezaji wa MKUHUMI. Kwa kuongeza uelewa kwa wanajamii na wanasiasa kuhusu manufaa yanayoweza kuletwa na MKUHUMI kwa jamii za vijijini, mpango huu una utashi wa kisiasa.
Hatari 6. Fedha za MKUHUMI kuto kutoa motisha ya kutosha kwa ajili ya usimamizi endelevu wa misitu.	Uwezekano wa kutokea: wa kati Athari zinazoweza kujitokeza kwa mradi : Kubwa	Kutafuta uhakiki kutoka CCB na VCS, lengo la mradi ni kupata bei ya hewa ukaa itakayotoa motisha ya kutosha kwa jamii kwa ajili ya kupunguza uharibifu wa misitu.

G 3.7 Uendelevu

Shughuli zote za utekelezaji wa kufanikisha MKUHUMI zitaongozwa na wanajamii. TFCG na MJUMITA, kwa kutumia fedha kutoka serikali ya Norway, wametumia miaka minne (2010 – 2013) kuwaandaa wanajamii kuendeleza majukumu ya uhifadhi wa misitu kupitia mafunzo na kuwezesha mipango ya matumizi bora ya ardhi, upatikanaji wa vyeti vya umiliki wa ardhi ya kijiji, kutatua migogoro ya mipaka ya vijiji, uanzishwaji wa usimamizi wa misitu ya jamii na kuwezesha mfumo madhubuti na unaofaa wa utekelezaji wa MKUHUMI.

G 3.8 Ushirikishaji wa wadau

Mfumo wa hatua-kwa-hatua wa utekelezaji wa mradi ulianzishwa uliozingatia kanuni za kupewa taarifa za kabla na kuwa na uhuru wa kutoa ridhaa au kukataa. Hatua hizo ni pamoja na:

- Mikutano ya utangulizi kwa Halmashauri za vijiji
- Kuelimisha jamii kuhusu mradi na majadiliano katika ngazi za vitongoji.
- Kuelimisha jamii, majadiliano na kuomba ridhaa ya jamii ya kutekeleza MKUHUMI katika mkutano wa Kijiji.
- Kufanya usanifu wa mradi katika ngazi ya jamii na tathmini ya athari za kijamii, warsha ya tathmini ya athari za kijamii ilifanyika ikijumuisha wawakilishi wa vijiji vinavyoshiriki mradi.
- Warsha kuhusu tathmini shirikishi ya athari za kijamii ilifanyika katika eneo la mradi kwa kuwahusisha wawakilishi na wadau wote wa eneo la mradi.
- Mikutano ya majadiliano na viongozi wa vijiji ilifanyika kuhusu mipango ya matumizi bora ya ardhi, usimamizi shirikishi wa misitu na MKUHUMI.
- Majadiliano na wanajamii kuhusu utaratibu wa utekelezaji wa shughuli za maandalizi ya MKUHUMI.
- Mipango ya matumizi bora ya ardhi, usimamizi wa misitu ya jamii na kuandaa sheria ndogo za kuratibu mgawanyo wa fedha za MKUHUMI viliyoandaliwa kwa kuongozwa na wanajamii.

- Majadiliano na wanajamii katika kupanga namna ya kufanya malipo ya fedha za MKUHUMI na kufanya majaribio ya malipo ya fedha za MKUHUMI.
- Majadiliano na tathmini ya utekelezaji wa mradi kwa kushirikisha wawakilishi wa jamii na wadau wengine.
- Kuelimisha jamii kuhusu utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji na mipango ya usimamizi wa misitu.
- Kujadiliana na kuandaa kwa njia shirikishi makubabaliano ya huduma za kitaalam za uuzaji wa hewa ukaa kati ya vijiji na MJUMITA.
- Mafunzo ya jamii kuhusu majukumu na wajibu.
- Majadiliano na jamii na kuomba kuwa na ridhaa ya maandishi ya kuendelea na utekelezaji wa MKUHUMI.

G 3.10 Utatuzi wa Migogoro

Utaratibu wa utatuzi wa migogoro inayotokana na utekelezaji wa MKUHUMI utafuata taratibu zilizopo katika Wilaya za kutatua migogoro mingine. Wawakilishi wa jamii walimchagua Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika kuwezesha utatuzi wa migogoro baina ya wanavijiji na wawezeshaji wa Mradi wa MKUHUMI.

G 4.6 Usalama wa Wafanyakazi

Kwa wanajamii, kuna tahadhari za hatari zinaweza kutokea kutokana na shughuli za doria ambazo mradi unaangalia namna ya kuzipunguza kwa kuhakikisha kuwa vikosi vya doria na kamati za maliasili wana vifaa vinavyohitajika.

G5 Hali ya Kisheria na Haki Miliki

G 5.1 Haki Miliki

Kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa MKUHUMI, MJUMITA na TFCG wamekuwa wakiwezesha wanavijiji kupata vyeti vya umiliki wa ardhi za vijiji vyao. Shughuli hii bado inaendelea kupitia Halmashauri za Wilaya na Serikali Kuu wanasubiriwa kukamilisha mchakato huo.

G 5.2 Kupitishwa kwa mradi na mamlaka husika

Mradi umepitishwa na Halmashauri za vijiji vyote vinavyotekeleza mradi. Ridhaa ya kuendelea kutekeleza MKUHUMI imetolewa na vijiji kupitia makubaliano yaliyofanyika baina ya Halmashauri za Vijiji na MJUMITA.

G 5.3 Kupewa taarifa za kabla na kuwa na uhuru wa kutoa ridhaa au kukataa

Kama inavyotakiwa kwa shughuli za maandalizi ya MKUHUMI, MJUMITA na TFCG wamejitahidi kuwa na utaratibu mzuri na wa mfano katika kutekeleza kanuni ya kupewa taarifa za kabla na kuwa na uhuru wa kutoa ridhaa au kukataa (angalia 3.8).

G 5.4 Kuhamisha makazi ya watu kwa lazima

Mradi haukuhitaji kuhamisha makazi ya watu kwa lazima kama njia itakayosaidia kupunguza hewa ukaa.

G 5.5 Shughuli zisizo halali

Shughuli zitakazokuwa kinyume na sheria ndogo za kijiji za usimamizi wa msitu wa hifadhi wa kijiji na zitaathiri tabianchi, jamii au athari za bionuwai zikijumuisha kuakata magogo au mbao bila kibali, uchomaji wa mkaa bila kibali, kuanzisha moto katika mradi na kufyeka msitu wa hifadhi wa kijiji kwa ajili ya shughuli za kilimo.

G 5.6 Hakimiliki ya hewa ukaa

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya 1999, misitu na rasilimali nyingine katika kijiji iko ndani ya mamlaka ya vijiji na wanajamii wana haki ya kunufaika na rasilimali hizo ikiwa ni pamoja na hewa ukaa.

SEHEMU YA TABIANCHI

CL1 Hali ya tabianchi bila mradi

Sehemu hii inatoa makadirio ya uzalishaji wa gesijoto katika eneo la mradi kwa kaungalia hali ya tabianchi bila mradi

CL 1.1 Makadirio ya uzalishaji wa gesijoto bila mradi

Ili kukadiria uzalishaji wa Gesi Joto bila mradi (hali ya awali), Mradi ulifuata hatua zilizoidhinishwa katika Kanuni za Viwango vya Hiari vya soko la koboni (VCS methodology VM0015)

Kwa kutumia picha za anga na takwimu za taarifa za kijiografia, mradi uliandaa ukanda rejea wa maeneo ya misitu ikiwemo misitu iliyoko ndani ya eneo la mradi na misitu mingine katika Wilaya ya Lindi and Ruangwa. Umakini ulitumika kuhakikisha kwamba ukanda rejea ulifanana na eneo la mradi hususan visababishi vya ukataji wa miti, muundo wa kijiografia, hali ya kiikolojia na hali ya kijamii na kiuchumi.

Tulipomaliza kuandaa ukanda rejea, uchambuzi wa historia ya ufyekaji wa misitu kutoka mwaka 2001 hadi 2012 ulifanyika ili kujua kiwango cha ufyekaji na mwenendo wa ufyekaji katika eneo la ukanda rejea. Mradi uligundua kwamba wastani wa kiwango cha ufyekaji kwa mwaka katika ukanda huu ni asilimia 1.99.

Mwenendo wa ufyekaji ukikusisha na sababu mbalimbali kama vile umbali na barabara, umbali na makazi, umbali na ufyekaji uliofanyika hivi karibuni, miteremko, n.k. zilitumika katika mfumo wa kompyuta ili kubashiri maeneo ambayo yanaweza kufyekwa katika eneo la ukanda rejea kwa miaka 10 ijayo. Mradi uliweka maoteo kwamba kiwango cha historia ya ufyekaji kitaendelea kwa kiwango kilekile. Ramani ya maoteo ya ufyekaji wa misitu iliwekwa juu ya ramani ya aina ya misitu mbalimbali ili kujua kiasi cha kila aina ya msitu ambacho kingefyekwa kwa kila mwaka katika hali ya awali.

Ili kujua kiasi cha uzalishaji wa Gesi Joto ambacho kingetokana na ufyekaji wa kila aina ya msitu mradi ulifanya kazi na wajumbe waliopewa mafunzo kutoka katika Kamati za Maliasili za vijiji kupima jumla ya masalia ya viumbe hai juu ya ardhi katika aina ya misitu mbalimbali. Maoteo yalifanyika kwa kuitumia kanuni za mlinganyo wa mahesabu zilizotengenezwa na watafiti kutoka Chuo Kikuu Cha Kilimo cha Sokoine (SUA) vilivyotumika kutafsiri vipimo vya vipenyo vya miti kutoka msituni kwenda katika makadirio ya jumla ya uzito wa masalia ya viumbe hai katika maeneo ya juu ardhi na chini ya ardhi. Wakati huo huo, mradi pia ulipima jumla yote au uzito wa masalia ya viumbe hai katika maeneo ambayo yalikuwa yamefyekwa takriban miaka 10 hadi 20 iliyopita ili kujua wastani wa kiasi cha hewa ukaa katika maeneo haya kitakachokuwepo baada ya ufyekaji. Sababu za uzalishaji wa gesi joto katika kila aina ya msitu inapatikana baada ya kupata tofauti kati ya wastani wa kiasi cha hewa ukaa baada ya ufyekaji wa aina ya msitu na kiasi cha hewa ukaa cha aina hiyo yam situ mwanzoni kabla ya ufyekaji.

Kuongezea katika uzalishaji wa hewa ukaa, kuchoma misitu pia kunaachia hewa chafu za methani na shura (nitrous) ambazo zinakaa kwa muda mfupi lakini ni gesijoto hatari zaidi ya kabondioksidi. Kwa kufuata kanuni hizi, mradi ulitumia sababu za uzalishaji zilizokadiriwa na Jukwaa la kimataifa la Mabadiliko ya Tabianchi (IPCC) ili kujua uzalishaji wa gesijoto wa hali ya awali ambao ungetokea kutokana na uchomaji wa maeneo ya misitu (kama sehemu ya kutayarisha mashamba).

Jedwali la kwanza hapa chini linatoa matokeo ya uchambuzi wa uzalishaji wa gesi joto ambao ungewezakutokea bila kuwepo kwa mradi.

Jedwali la 3: Mabadiliko ya kiasi cha hewa ukaa katika hali ya awali na uzalishaji wa gesijoto kutokana na uchomaji wa misitu bila uwepo wa mradi.

Mwaka Mradi wa t	Mabadiliko ya kiasi cha hewa ukaa katika hali ya awali		Uzalishaji wa gesijoto katika hali ya awali	
	Kwa mwaka	Kwa kulimbikiza	Kwa mwaka	Kwa kulimbikiza
	ΔCBSLPA_t	ΔCBSLPA	EBBSLPA_t	EBBSLPA
	Makadirio ya tani ya hewa ukaa ($\text{tCO}_2\text{-e}$)	Makadirio ya tani ya hewa ukaa ($\text{tCO}_2\text{-e}$)	Makadirio ya tani ya hewa ukaa ($\text{tCO}_2\text{-e}$)	Makadirio ya tani ya hewa ukaa ($\text{tCO}_2\text{-e}$)
1	-126,560	-126,560	9,905	9,905
2	-114,024	-240,583	8,866	18,771
3	-112,758	-353,341	8,713	27,484

4	-113,212	-466,553	8,695	36,179
5	-108,057	-574,610	8,239	44,418
6	-104,407	-679,017	7,903	52,321
7	-99,345	-778,362	7,458	59,779
8	-100,788	-879,150	7,524	67,303
9	-97,697	-976,847	7,235	74,537
10	-95,765	-1,072,612	7,038	81,575

CL 2. Athari chanya halisi za tabianchi

Mradi utapunguza kiwango cha uzalishaji wa gesijoto katika eneo la mradi kwa kipindi cha utekelezaji wa mradi.

CL 2.1. Makadirio ya uzalishaji wa gesijoto katika eneo la mradi

Ili kukadhiria uzalishaji unaoweza kutokea katika hali ya kuwepo kwa mradi, mradi ulitaka kujua ufanisi utakaokuwepo kwa kupunguza ufyekaji wa misitu katika kipindi cha kwanza cha miaka 10 ya mradi. Mradi ulikuwa na maoteo kwamba ufanisi ungeweza kuongezeka kadri ya muda unavyoenda. Hata hivyo, kwa sababu wanavijiji waliacha maeneo makubwa ya misitu nje ya hifadhi za misitu, mradi ulidhani ufanisi hautoweza kufika asilimia 100. Mradi ulikadiriya ufanisi wa kuanzia asilimia 30 na baada ya hapo kuongezeka kwa ufanisi kwa asilimia 5 kila mwaka hadi miaka 7, ambapo kiwango cha juu cha ufanisi kitafikia asilimia 60 kitafikiwa (hapo mradi ungeweza kupunguza kiwango cha uzalishaji cha hewa ukaa kwa asilimia 60). Kwa sababu mradi hauzalishi gesijoto ya aina yeyote ambayo haitakuwepo katika hali ya awali, ili kujua uzalishaji katika kipindi cha kuwepo kwa mradi, mradi uliamua kupunguza kiwango cha uzalishaji katika hali ya awali kwa kutumia kiwango cha ufanisi kilichokadiriwa kwa kila mwaka kwa miaka 10 ya mwanzo ya mradi. Kiashiria kilekile cha kiwango cha ufanisi kilitumika katika mabadiliko ya kiasi cha hewa ukaa na uzalishaji usiokuwa wa hewa ukaa unaotokana na uchomaji wa misitu. Angalia jedwali la 2 na Jedwali la 3 kwa ajili ya matokeo.

Jedwali la 4: Makadirio yanayotarajiwa ya uzalishaji katika kipindi cha mradi kutokana na kupunguza kiasi cha hewa ukaa.

Mwaka wa Mradi wa t	Uzalishaji wa kiasi cha hewa ukaa katika hali ya awali	Kiashiria cha Ufanisi	Jumla ya kiasi cha hewa ukaa kilichopunguzwa kutokana na ufyekaji wa misitu uliyoepukwa na ambao haukupangwa	
	Kwa mwaka	Kwa mwaka	Kwa mwaka	Kwa kulimbikizwa
	$\Delta CBSL_t$	EI	$\Delta CUDdPA_t$	$\Delta CUDdPA$
	tCO ₂ -e	%	tCO ₂ -e	tCO ₂ -e
1	-126,560	30	-88,592	-88,592
2	-114,024	35	-74,116	-162,707
3	-112,758	40	-67,655	-230,362
4	-113,212	45	-62,266	-292,628
5	-108,057	50	-54,028	-346,657
6	-104,407	55	-46,983	-393,640
7	-99,345	60	-39,738	-433,378
8	-100,788	60	-40,315	-473,693
9	-97,697	60	-39,079	-512,772
10	-95,765	60	-38,306	-551,078

Jedwali la 5: Makadirio yanayotarajiwa ambayo yana uzalishaji wa mradi unaotokana na uchomaji wa misitu.

Mwaka wa Mradi wa t	Uzalishaji usiokuwa wa hewa ukaa katika hali awali	Kiashiria cha Ufanisi	Jumla ya uzalishaji usiokuwa wa hewa ukaa halisi wa makadirio yanayotarajiwa unaotokana na uchomaji wa misitu katika eneo la mradi	
	Kwa mwaka	Kwa mwaka	Kwa mwaka	Kwa kulimbikizwa
	$EBBBSPA_t$	EI	$EBBPSPA_t$	$EBBPSPA$
	tCO ₂ -e	%	tCO ₂ -e	tCO ₂ -e
1	9,905	30	6,933	6,933
2	8,866	35	5,763	12,696
3	8,713	40	5,228	17,924
4	8,695	45	4,782	22,706
5	8,239	50	4,119	26,826
6	7,903	55	3,556	30,382
7	7,458	60	2,983	33,365
8	7,524	60	3,010	36,375
9	7,235	60	2,894	39,269
10	7,038	60	2,815	42,084

CL2.2. Athari halisi za mradi ni chanya

Athari halisi na chanya za tabia nchi za mradi zilikadiriwa kwa kupata tofauti kati ya makadirio ya yanayotarajiwa ya uzalishaji katika kipindi cha mradi na makadirio yanayotarajiwa ya uvujaji kutokana na uzalishaji wa awali (angalia sehemu ya CL3). Matokeo yamewasilishwa katika jedwali la 4

Jedwali la 6: Makadirio yanayotarajiwa ya Kiasi halisi cha makadirio ya upunguzaji wa uzalishaji wa gesi joto kutokana na shughuli za mradi.

Mwaka	makadirio ya upunguzaji wa uzalishaji wa gesi joto au utoaji wa (tCO ₂ e)
2012-2013	33,980
2013-2014	35,699
2014-2015	40,328
2015-2016	45,532
2016-2017	48,263
2017-2018	51,270
2018-2019	53,188
2019-2020	53,939
2020-2021	52,256
2021-2022	51,196
Jumla ya makadirio ya Upunguzaji wa gesi	465,651
Jumla ya idadi ya miaka ya uuzaji	10
Wastani wa mwaka wa Upunguzaji wa gesi	46,565

CL 3. Uvujaji

Uzalishaji wa gesijoto nje ya eneo la mradi unaosababishwa na shughuli za mradi unafanyiwa tathmini na kupunguzwa ili kupata matokeo chanya ya tabianchi.

CL 3.1. Aina ya uvujaji na eneo la uvujaji

Kutokana na matokeo ya historia ya ufyekaji katika eneo la ukanda rejea na uelewa wa wanavijiji katika eneo la mradi, mradi uligundua kuwa uvujaji ungetokea zaidi ndani ya eneo la kilometa 6.1 la eneo la mradi. Kama sehemu ya mkokotoo wa uzalishaji wa awali, mradi pia ulikokotoa uzalishaji wa hewa ukaa katika ukanda ya uvujaji. Wakati wa mradi, ufyekaji wa misitu utafuatiliwa katika eneo la mradi. Kama ufyekaji zaidi umeonekana katika ukanda wa uvujaji kuliko ulivyobashiriwa wakati wa hali bila mradi, inamaana ufyekaji huo utachukuliwa na uvujaji.

CL 3.2. Njia za kupunguza uvujaji

Mradi umetekeleza shughuli mbalimbali na wanavijiji zilizolenga kupunguza uvujaji. Shughuli muhimu zaidi za kupunguza uvujaji zaidi ni kuhamasisha kilimo bora ambacho kitapunguza mahitaji ya wakulima katika eneo la mradi kufyeka maeneo mapya kwa ajili ya mashamba. Mradi pia unahamasisha kilimo bora katika vijiji vya jirani kwa sababu ufyekaji mwingine katika eneo la mradi katika hali ya bila mradi ungesababishwa na watu kutoka katika vijiji vya jirani.

CL3.3. Kupunguza Uzalishaji wa gesijoto zisizo hewa ukaa

Mradi hautegemei kupunguza sana uzalishaji wa gesijoto zisizo hewa ukaa ambao ungechukuliwa kama uvujaji. Mathalan, mradi haujajishugulisha na ufugaji wa mifugo, ambayo kama ni kwa wingi unaweza kusababisha uzalishaji wa gesi ya metahni na shura.

CL 4. Ufuatiliaji wa athari za tabianchi

Ufuatiliaji wa athari za tabianchi utafanya tathmini katika eneo la mradi na nje ya eneo la mradi.

CL4.1. Mpango wa ufuatiliaji wa athari za tabianchi

Mradi utafanya ufuatiliaji wa ufyekaji wa misitu angalau mara moja kila miaka miwili kwa kutumia picha za anga zinazopatikana kwa urahisi kama vile Landsat. Pale itakapowezekeana, mradi utajaribu kufuatilia ufyekaji wa misitu kila mwaka. Maeneo yoyote ambayo ufyekaji utabainika yatatandaziwa juu ya ramani ya aina ya misitu hiyo ili uzalishaji wa hewa ukaa kutoka aina hii ya misitu uweze kutambuliwa.

Mara moja katika kila miaka mitatu hadi mitano, (3-5), mradi pia utashirikiana na wajumbe wa kamati za maliasli za vijiji waliopewa mafunzo kupima kiasi cha hewa ukaa kwa kutembelea tena vitalu vya hewa ukaa vilivyotengenezwa wakati wa mwanzo wa mradi. Kwa sababu wanavijiji wanalinda misitu katika eneo la mradi na sehemu kubwa ya misitu ilikuwa haijafika asilimia 100 ya ukomavu, itatarajiwa kwamba mradi utapata nyongeza ya kiasi cha kaboni muda unavyoenda. Mabadiliko katika kiasi cha kaboni yatatumika kutoa taarifa za makadirio ya uzalishaji wa awali kwa ajili ya miaka kabla ya uchambuzi.

CL4.2. Usambazaji wa mpango na taarifa za ufuatiliaji

Tathmini ya ufyekaji wa misitu ulifanyika kila baada ya kipindi kisichopungua miaka miwili (2), na matokeo yake yatawasilishwa kwa kila kijiji kinachotekeleza mradi. Taarifa za sehemu ambayo ufyekaji umefanyika katika kila kijiji zitatolewa kwa Kamati za Maliasili za kila kijiji ili kubaini nani wanaohusika na kuhakikisha uharibifu haundelei. Matokeo ya tathmini ya uharibifu wa misitu yatawasilishwa katika mkutano mkuu wa kijiji wa kujadili masuala ya MKUHUMI ili wanavijiji waelewe namna walivyofanikiwa kupunguza kiwango cha uharibifu wa misitu ukilinganisha na kiwango cha awali na kiwango cha malipo walichopata kutokana na mauzo ya hewa ukaa.

SEHEMU YA JAMII

CM1 Athari Chanya Halisi za Jamii

CM 1.1 Makadirio ya athari za jamii

Athari zinazokadiriwa kwa jamii kutokana na mradi zimeorodheshwa hapa chini kulingana na malengo yafuatayo:

CM Lengo la Kijamii 1. Kudumisha huduma za mfumo ikolojia ya misitu na upatikanaji endelevu wa mazao ya misitu kupitia mfumo wenye usawa na madhubuti wa usimamizi shirikishi wa misitu..

Athari ya Kijamii (CM) 1. Misitu inayomilikiwa na jamii itasimamiwa kwa njia shirikishi, madhubuti na yenye usawa.

Athari ya Kijamii (CM) 2. Mazao ya misitu yataendelea kupatikana na kuwafikia wanajamii wote pamoja na kaya maskini kwa namna zilizokubalika kwa njia shirikishi.

Athari ya Kijamii (CM) 3. Vijiji vitaongozwa vizuri zaidi.

Athari ya Kijamii (CM) 4. Wanajamii watakuwa na mfumo salama wa umiliki wa ardhi.

Athari ya Kijamii (CM) 5. Vyanzo vya maji vitalindwa vizuri zaidi

Athari ya Kijamii (CM) 6. Mmomonyoko wa udongo utapungua

Lengo (CM) 2. Kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja kutokana na MKUHUMI kwa kuwekeza katika shughuli za kilimo bora na shughuli nyingine za kiuchumi kwa kuboresha hali ya ujumla ya maisha na kulenga zaidi kaya maskini na akina mama.

Athari ya Kijamii (CM) 7. Pato la mtu mmoja mmoja litaongezeka na vyanzo vya mapato vitaongezeka kwa kulipwa fedha za MKUHUMI.

Athari ya Kijamii (CM) 8. Wakulima wanawake na wanaume, ikiwa ni pamoja na wanaotoka katika kaya maskini, wataanza kutumia mbinu za kilimo bora chenye faida zaidi, endelevu na kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi na watawekeza katika shughuli nyingine za kiuchumi na/au mbinu za kuongeza thamani ya mazao.

CM Lengo 3. Kuongeza ubora na upatikanaji wa huduma za jamii na miundombinu.

Athari ya Kijamii (CM) 9. Mapato yanayotokana na MKUHUMI yatachangia kuimarisha huduma za jamii na miundombinu.

Athari ya Kijamii (CM) 10. Vijiji vitakuwa na majengo ya ofisi

CM2. Athari kwa wadau walio nje ya eneo la mradi

CM 2.1 Athari hasi zinazotegemewa kwa wadau walio nje ya eneo la mradi na CM 2.2 Kupunguza athari zinazotegemewa kwa wadau walio nje ya eneo la mradi

Wakulima wachache kutoka katika vijiji viwili vilivyo katika eneo lililo nje ya mradi: Chikonji na Kilangala wanaweza kuathirika na vizuizi vya ufyekaji wa misitu. Kama sehemu ya shughuli za maandalizi ya utekelezaji wa MKUHUMI, MJUMITA wamekuwa wakitoa mafunzo kuhusu kilimo hifadhi katika vijiji hivi.

CM 2.3 Athari hasi kamili kwa wadau wengine

Hakuna athari iliyotegemewa

SEHEMU YA BIONUWAI

B1 Athari Chanya halisi za Bionuwai

B 1.1 Manufaa halisi ya bionuwai

B Lengo 1. Kuhifadhi aina za viumbe vilivyo katika tishio na hatari ya kutoweka.

B Athari 1. Idadi ya viumbe vilivyo katika tishio na hatari ya kutoweka vinaendelea kuwepo katika eneo la mradi.

B Lengo 2. Kuhifadhi eneo la nyongeza la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

B Athari 2. Eneo la nyongeza la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki kuendelea kuwepo katika eneo la mradi.

B Athari 3. Kuna msukumo mdogo wa ufyekaji wa misitu na uharibifu wa misitu katika eneo la misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki.

B Athari 4. Jamii na wadau wanajihusisha kikamilifu katika usimamizi wa misitu ya pwani ya ukanda wa Afrika Mashariki katika eneo la mradi.

B 1.2 Athari hasi kwa thamani kubwa ya uhifadhi:

Hakuna athari hasi inayotegemewa.

B 1.3 Aina ya viumbe (mimea) vamizi: Hakuna viumbe vamizi vinavyotegemewa vilivyoingia kwenye eneo la mradi.

B 1.4 Madhara hasi ya viumbe visivyo vya eneo husika: Hakuna madhara yanayotemewa ya viumbe visivyo vya eneo husika.

B 1.5 Hakuna viumbe vya vinasaba: Hakuna viumbe vya vinasaba vilivyotumika.

B2. Athari za bionuwai katika eneo la nje ya mradi

B 2.1 Athari hasi za bionuwai zinazotarajiwa katika eneo la nje ya mradi na B 2.2 Kupunguza athari hasi za bionuwai zinazotarajiwa katika eneo la nje ya mradi

Hakuna athari hasi za bionuwai zinazotarajiwa katika eneo la nje ya mradi.

SEHEMU YA KIWANGO CHA DHAHABU

GL 1 Manufaa ya Kuhimili mabadiliko ya Tabia Nchi

GL 1.1 Athari za mabadiliko ya tabianchi ya kanda/mkoa na GL 1.3 Athari za mabadiliko ya tabianchi za eneo la mradi

Kwa ujumla, hali ya tabianchi ya Tanzania inaendelea kuwa haitabiriki kutokana na kuongezeka kwa matukio ya upepo mkali, ukame na mafuriko. Utabiri wa hali ya tabianchi unaonesha ongezeko la mvua katika miezi ya Desemba – Januari- Februari, wakati Machi-Aprili-Mei hupokea kiasi kidogo cha mvua; na huongeza joto katika eneo lote la mashariki mwa Tanzania, hususan katika kipindi cha baridi cha Julai-Agosti.

GL 1.2 Hatari ya Mabadiliko ya Tabianchi

Ukuaji hafifu wa mazao na kushuka kwa kiwango cha uzalishaji kunaweza kuongeza umaskini na mzunguko tata wa kuongezeka kwa hali ya mazingira magumu yanayotokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi. Kuongezeka kwa umaskini na upatikanaji wa maji wa msimu, migogoro inaweza kuongezeka na kupelekea kushindwa kuimarisha utawala bora.

GL 1 Shughuli za hiari

GL 1.4 Shughuli za mradi kusaidia jamii kuhimili mabadiliko ya tabianchi

Mafunzo yalitolewa kwa wanajamii kuhusu shughuli za kilimo bora hususan kulenga mbinu za kilimo zitakazomwezesha mkulima kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

GL2 Manufaa ya pekee kwa Jamii

GL 2.1 Nchi yenye maendeleo hafifu ya watu

Kwa mujibu wa Taarifa ya Maendeleo ya Watu 2013 ya UNDP, Tanzania ipo miongoni mwa nchi yenye maendeleo hafifu ya watu.

GL 2.2 Athari kwa kaya maskini zaidi, GL 2.3 Mtiririko wa manufaa kwa kaya maskini na na GL 2.4 Athari kwa kaya maskini

Kaya zote ikiwa ni pamoja na zote zilizo katika kundi maskini kabisa miongoni mwa jamii watapokea malipo ya MKUHUMI kwa kuzingatia mfumo wa malipo wa mradi. Kaya zote zitaweza kufikiwa na miundombinu bora na kupata huduma kutokana na miradi ya maendeleo inayogharamiwa moja kwa moja au kwa sehemu na fedha za MKUHUMI.

GL3 Manufaa ya pekee kwa bionuwai

GL 3.1 Hali ngumu ya maisha

Mradi wa MKUHUMI unategemea kuleta ahueni dhidi ya hali ngumu ya maisha kwa kutekeleza mfumo wa mgawanyo wa fedha unaozingatia usawa kwa wakaazi wote wa kijiji na kaya maskini.

GL 3.2 hali ya kutokuwepo kwa mbadala

Mtawanyiko unaojulikana wa galago wa Rondo ni kilometa za mraba 92.6 za msitu katika misitu sita ya ukanda wa pwani. Pamoja na kuwa hakuna takwimu zilizopo kuhusu uwingi wao katika kila eneo, kuna uwezekano mkubwa kuwa Miinuko ya Noto inaweza kuwa na zaidi ya asilimia 10 ya uwingi wao duniani.